# Jarida la UQAB

Toleo 9
Oktoba 2017 Miladi
Muharram 1439 Hijriya

Hakuna Haki Ndani ya Nidhamu Dhalimu ya Demokrasia

Rohingya: Jeshi Lazima Lichangamke!

Je, Kazi ya Kusimamisha Tena Khilafah Imefikia Wapi?

Ni Nani Atakaye Komesha Mauaji ya Halaiki Dhidi ya Waislamu wa Rohingya

Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi -Halaqa 5

SWALI / JAWABU: Mkakati wa Amerika Nchini Afghanistan




## Mtandao wa YouTube ni Mshirika wa Bashar Katika Uhalifu Wake




# Mtandao wa YouTube ni Mshirika wa Bashar Katika Uhalifu Wake

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Idara ya mtandao wa YouTube imefuta maelfu ya video zinazo onyesha uhalifu wa katili wa Sham tangu kuanza kwa mapinduzi nchini Syria. Mnamo 24/08/2017, mtandao huu ulifunga pia vituo vyetu viwili: HT Media – tovuti mbadala, na tovuti ya Khilafah. Na mnamo 09/09/2017, ilifunga kituo cha Nidaat Al-Aqsa, baada ya kufunga vituo vyetu vinne vyengine awali kati mwezi uliopita. Mtandao huu ulihalalisha hatua hii kwa kisingizio cha haja ya kupambana na ugaidi!

Katika majaribio ya kutapatapa na yasiokuwa na maana, mtandao huu ulijaribu kuhalalisha uhalifu wake kwa kuonyesha kuwa huku si kugandamiza uhuru wa kujieleza bali hili ni jaribio la kutetea maadili ya hadhara ya kimagharibi. Mtandao huu unadai kuwa hautaki kusaidia katika kazi ya wale wanao shambuli maadili ya jamii ya kimagharibi inayo tukuza uhuru wa kujieleza na uhuru wa rai! Mtandao unaeleza katika mwisho wa taarifa yake iliyotolewa na mtandao huo: "Watu walio vuka mipaka na magaidi wanataka kushambulia na kumomonyoa sio tu usalama wetu bali pia maadili yetu, ambayo ndio mambo yanayo zifanya jamii zetu kuwa wazi na huru. Hatupasi kuwaacha wafanye hivyo". (Angalia taarifa hiyo ya mtandao wa YouTube: https://www.blog.google/topics/google-europe/four-steps-were-taking-today-fight-online-terror).

Hivyo basi, uhalalishaji huu ovyo umefichuliwa na mtandao huu kwa kupitia kuchanganya baina ya matendo ya kimada yanayo lenga raia, na mdahalo wa kifikra na kisiasa kwa kile wanacho kiita "maadili" ya jamii ya kimagharibi. Sasa kitendo hiki kitaoanishwa vipi na madai yao ya kirongo kwamba maadili ya kimagharibi, yametokana na msingi wa kidemokrasia, ambao ni msingi huo huo pia unatukuza uhuru wa kibinafsi, ikiwemo uhuru wa fikra, rai na kujieleza, inayo jumuisha pia kueleza rai zinazo pingana na kugongana, ima kupitia vyombo vya utawala, vyombo vya habari au vyenginevyo?!

Linalo maanishwa pekee na taarifa hii ni kukubali wazi wazi kuwa nyumba ya demokrasia ni hafifu zaidi kuliko nyumba ya buibui. Haiwezi kuhimili hijab (Khimar) inayovaliwa na mwanamke wa Kiislamu, wala kusikiza fikra kinzani inayo yajadili maelezo ya kirongo iliyo jengwa juu yake.

Pengine bwana Francis Fukuyama na wenzake, wasomi wa Kiamerika, washirika katika taarifa ya wasomi 60 waliyoitoa chini ya anwani "Kile Tunacho Pigana Nacho" mwanzoni mwa 2002 kuhalalisha vita vya msalaba vilivyo anzishwa na George Bush dhidi ya Ummah wa Kiislamu, ikidai kuwa maadili haya ni ya wanadamu ulimwengu mzima, kama vile Fukuyama alivyodai kwa kuiita harakati ya mwisho wa historia kutokana na ushindi wa ule unaoitwa mfumo wa kidemokrasia (dhidi ya ukomunisti mnamo 1991). Pengine, ikiwa wana chembe ya ikhlasi ndani ya nafsi zao kwanza kisha kwa watu wao wenyewe, basi watatambua ukweli kuwa maelezo ya demokrasia "yanayo kinaisha" pekee ni utumiaji nguvu wazi unaotokana na sheria ya kimwitu na wala sio kutokana na ithibati yoyote ya kifikra wala ya kisomi. Alhamdulillah, ukweli wa vita vya msalaba vya kimagharibi dhidi ya Waislamu umefichuka kwa kila aliye na macho, kwani sio siri tena; kulindwa kwa wamagharibi, wakiongozwa na Amerika – mmiliki wa sanamu ya Uhuru, kuilinda kwao Sham kutokana na uhalifu wake ambao ni fedheha kwa wanadamu kila wakati na mahali walipo.

Tunatamatisha kwa kusema kuwa uhalifu wa mtandao wa YouTube wa kuficha uhalifu wa katili wa Damascus hauta tuzuia sisi kuendelea na kazi ya kuangamiza ukatili wake na kuuondoa uhalifu wake, huku tukitambua wazi kuwa hili litafanyika pekee kupitia kusimama kwa serikali ya Khilafah katika njia ya Utume, iliyo na uwezo wa kuzizuia serikali za kikoloni kutokana na lengo lao.

إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعَالَمِينَ وَلَتَعْلَمُنَّ نَبَأَهُ بَعْدَ حِينٍ

**Haya kuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote. Na bila shaka mutajua habari zake baada ya muda.** [Sad: 87-88]

**Dkt. Osman Bakhach**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Hakuna Haki Ndani ya Nidhamu Dhalimu ya Demokrasia




**Habari:**

Mnamo tarehe 1 Septemba 2017, mahakama ya juu ya Kenya ikiongozwa na jaji mkuu David Maraga akiwa na jopo la majaji sita walitoa uamuzi uliopelekea kufutiliwa mbali kwa matokeo ya kura za uraisi na hivyo basi kupelekea kubatilisha kutangazwa kwa Uhuru Kenyatta kama raisi mteule. Kati ya majaji sita, wanne walisema kuwa baada ya kuzingatia ushahidi kwa uamuzi wa walio wengi: kifungu 10, 38, 81 na 86 vya katiba na sehemu ya 39(1), 44 (a) na 83 za sheria ya uchaguzi, mtuhumiwa wa kwanza (tume ya IEBC) alifeli, alipuuza na alikataa kusimamia uchaguzi kwa njia na maelekezo ya katiba. Hukumu hii iliitaka tume ya IEBC kufanya uchaguzi mpya ndani ya siku 60. Raila Odinga alisema kuwa haki imetendeka na uamuzi huu ni kielelezo kwa Afrika.

**Maoni:**

Uamuzi huu wa mahakama ni njama nyengineyo ya walinganizi wa demokrasia kuiokoa nidhamu ya kidemokrasia kutokana na kuporomoka kwake, ambayo tangu 2007 imefeli kutambua 'uwezo' wa watu kupitia kura. Walifanya kampeni za kiwango kikubwa kwa kutumia kila aina ya khiyana kuhakikisha kuwa mabadiliko watakayo leta ni ya kisanii kwa jina la 'demokrasia komavu'; kubuniwa kwa cheo cha Waziri Mkuu kwa Raila Odinga na hatimaye kuapishwa kwake mnamo Aprili 2008 ili kumuwezesha kufikia uongozi kwa niaba ya Amerika. Wakaamsha hekaya ya ICC mnamo 2009 kutoa sura ya kujitolea kwa jamii ya kimataifa katika kujali amani na kumakinisha demokrasia nchini Kenya; na kupitishwa kwa katiba mpya ya 2010 kutoa fursa ya kutatua changamoto za kikatiba zilizo shuhudiwa katika katiba ya zamani.

Haya ni baadhi tu ya mabadiliko hadaifu waliyo yafanyia kazi, lakini kwa kuwa demokrasia yenyewe kama nidhamu ya utawala imechukuliwa kutoka katika mfumo batili wa kirasilimali. Mfumo batili ulio chipuza kutokana na akili finyo za watu lengo lake likiwa ni kutenganisha dini na maisha; hivyo basi hainge tarajiwa kutoa suluhisho ya kikweli kwa masuala yanayo wakumba wanadamu nchini Kenya na ulimwengu kwa jumla. Kwa kuwa mabadiliko hayo yalitokana na msingi wa fikra ya maslahi inayolenga kumnufaisha mteja mkuu. Zaidi ya hayo, hukumu hii inathibitisha yafuatayo:

1. Uhuru wa tume ya uchaguzi ya Kenya IEBC unatiliwa shaka ikiwa inashindwa na hata kuiweka mitambo yake humu nchini na badala yake kuamua kuiweka katika eneo la bwana wake wa kikoloni (Ulaya)!
2. Dori ya waangalizi wa uchaguzi ni kufuatilia uchaguzi huku wakiwa tayari wamejenga fikra ya matokeo yake na hatimaye kutoa ripoti za kumpendelea bwana wao anaye walipa kama ilivyo jitokeza kwa waangalizi wa uchaguzi kutoka Jumuia ya Nchi za Madola, Umoja wa Ulaya, IGAD walio muunga mkono kibaraka wa Uingereza Uhuru Kenyatta huku wale wa taasisi ya Carter Center wakimuunga mkono kibaraka wa Amerika Raila Odinga. Haya yamedhihirishwa kutokana na wengi wao kuuidhinisha uchaguzi huu kuwa wa sawa isipokuwa taasisi ya Carter Center, iliyo sema katika taarifa yake ya mnamo Agosti 10 kuhusu uchaguzi, iliungama kuwa "siku ya uchaguzi mipangilio ya upigaji na kuhesabu kura ilikuwa shwari lakini uwasilishaji matokeo kupitia njia ya kielektroniki haukuwa wa kuaminika."
3. Makampuni ya kimataifa yanajali sana uchumi wao kiasi kwamba walishughulishwa sana na hali ya utulivu nchini Kenya dhidi ya wito wa uchaguzi wa haki na hatimaye kutoa pongezi kwa Uhuru Kenyatta kwa kuchaguliwa tena licha ya kuwepo na tetesi za kutoridhika zilizotoka upande wa upinzani uliodai kuwa kulikuwepo na dosari za wazi katika uchaguzi huo.

Kupatikana kwa mabadiliko ya kweli ni kwa kupitia tu kubeba na kulingania mfumo badala pekee, unaotoka kwa Muumba wa wanadamu Anaye yajua maslahi yao. Mfumo huo ni Uislamu na kutawalishwa kwake ni hakikisho la kweli kwa amani, utulivu na mafanikio.

**Imeandikwa na Ali Nassoro**
**Kwa Ajili ya Afisi ya Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Rohingya: Jeshi Lazima Lichangamke!



**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**


Hizb ut Tahrir / Malaysia ilifanya jumuiko la amani na kutoa wito katika eneo la Msikiti wa Wilayah, jijini Kuala Lumpur, punde tu baada swala ya Ijumaa mnamo 15/06/2017 kuhusiana na mgogoro wa Rohingya. Mateso na mauaji yaliyo fanywa hivi karibuni na serikali ya Myanmar na magaidi wa kibudha juu ya Waislamu wa Rohingya eneo la Arakan ni ya kinyama kupita kiasi, yakidhihirisha uadui wao mkubwa na chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu. Katika wito huu, Hizb ut Tahrir inasisitiza kuwa tatizo la Waislamu wa Rohingya halita tatuliwa kupitia mashirika ya kiulimwengu kama Umoja wa Mataifa (UN), Shirika la Ushirikiano wa Nchi za Kiislamu (OIC) au Shirikisho la Mataifa ya Kusini Mashariki mwa Asia (ASEAN). Mgogoro wa Waislamu wa Rohingya pia hauta tatuliwa kupitia msururu wa usanii na maneno matupu ya viongozi wa Waislamu.

Hizb ut Tahrir inaliangalia suala hali kwa mitazamo miwili nayo ni wa muathiriwa na zimwi. Kwa mtazamo wa waathiriwa hawa, ndio, wanahitaji misaada ya kibinadamu, lakini kwa mtazamo wa mazimwi haya, majeshi ya Kiislamu ni lazima yaingie na kuyamaliza. Maadamu zimwi hili halijamalizwa, daima muathiriwa ataendelea kuwepo. Kuliondoa zimwi hili ndio njia pekee ya kuitatua kadhia hii kikamilifu na Jihad katika njia ya Allah ndio njia pekee ya kujibu maovu na ukatili wa zimwili hili. Kwa hakika, hakuna njia nyengine za kuwaokoa Waislamu eneo la Arakan kutokana na madhila, mateso na mauaji haya yasokwisha isipokuwa majeshi ya Kiislamu yatangaze Jihad kwa makafiri wa Myanmar.

Hizb ut Tahrir inatoa wito kwa Ummah wa Kiislamu kuunganisha sauti zao na kupambana kuuonyesha ulimwengu kwa jumla na Myanmar haswa, kuwa Waislamu ni Ummah mmoja na hawata nyamazia kimya yale yanayo wakumba ndugu zao. Hizb ut Tahrir haita sitisha ulinganizi wake na itaendelea kufanya kazi mpaka majeshi ya Kiislamu yapelekwe au Khilafah katika njia ya Utume isimamishwe, itakayo waokoa Waislamu wa eneo la Arakan na kuipa funzo serikali ya Myanmar. Katika ulinganizi wake, Hizb ut Tahrir inasisitiza kuwa hatuwezi tena kuweka matumaini yetu kwa watawala, lakini tuna matumaini kuwa majeshi ya Waislamu yaliyo na ikhlasi yanayo tambua majukumu yao, yataanzisha Jihad dhidi ya serikali ya Myanmar.

Pasi na shaka, tuna hitaji sana serikali ya Kiislamu itakayo tawaliwa na Khalifah kwa al-Quran na al-Sunnah, Khalifah ambaye InshaAllah atalipeleka jeshi na kuanzisha Jihad katika njia ya Allah kuwaokoa Waislamu wote wanao dhulumiwa katika kila sehemu ya dunia. Kwa hakika, Khilafah itamaliza ukatili na ukafiri na kubadilisha mateso na giza kuwa mafanikio, nuru na rehma kwa wanadamu. Enyi Waislamu, njooni muungane na Hizb ut Tahrir! Tuunganisheni sauti zetu tupambane kwa ajili ya kheri ya Ummah huu na kwa ajili ya kheri yetu wenyewe hapa duniani na kesho Akhera. Kusimamisha Khilafah ni faradhi na kwa matakwa ya Allah, Khilafah al-Rashidah ala Minhaj Nubuwwah karibuni itarudi tena kutawala ulimwengu kwa mara ya pili.

**Abdul Hakim Othman**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir Malaysia**



# Je, Kazi ya Kusimamisha Tena Khilafah Imefikia Wapi?

Pindi Allah (subhanhu wata'ala) alipo taka kuinusuru dini yake, Uislamu, Yeye (subhanhu wata'ala) alifungua njia ya kuibuka kwa dola ya Kiislamu mjini Al Madinah kupitia kuzifanya hali za ndani na nje kuwa tayari kwa mazazi yake.

Kuhusu hali ya ndani, A'ishah, (ra) ameripotia kuwa Allah (subhanhu wata'ala) alifungua njia ya ushindi kwa dini yake kupitia vita vya Bua'ath vilivyo pelekea vifo vya viongozi wakongwe wa makabila ya Al-Aws na Al-Khazraj; tofauti na Makkah na Taif.

Kuhusu hali za nje, kulikuweko na mgogoro baina ya Ufalme wa Kifursi na Ufalme wa Kirumi. Zaidi ya hayo, kulikuweko na ufisadi, dhulma na umasikini yaliyo sababishwa na dola hizo.

Ingawa mazazi ya Khilafah leo yanatarajiwa wakati wowote chini ya hali yoyote ya kieneo au ya kimataifa, mtu anaweza kushangazwa na matukio ambayo Allah (subhanhu wata'ala) anayatumia kutoa mwanya wa kuzaliwa tena Khilafah. Matukio haya na hali hizi yanajumuisha (1) kuanguka kwa maadui zetu, (2) kuamka kwa Umma wa Kiislamu, na (3) maendeleo ya Hizb ut Tahrir ("Hizb").

Makala haya yamekusudia kuelezea nukta hizi tatu kwa ufafanuzi; na wala hayakusudii kuchambua Aya na Hadith zinazo toa bishara njema ya kurudi kwa Khilafah.

Ama kuhusu kuanguka kwa maadui zetu:

Waandishi wengi, kama Noam Chomsky na Emmanuel Todd, walianza kuiita Amerika "mtu mgonjwa" na wengine wakaanza kuzungumza wazi wazi kuhusu kuporomoka kwa Amerika na kujadiliana kuhusu hali ya kisiasa baada ya ufalme wake. Hii ni kutokana na yafuatayo:

1. Magharibi, na hususan Amerika, imekengeuka kutoka katika shina la mfumo wa urasilimali ambapo miito ya uhuru, haki za kibinadamu na demokrasia imeonekana kuwa feki. Kwa mfano:

(a) Mauaji ya watoto nusu milioni wa Iraq mnamo 1991, bila ya kutaja mamilioni ya wanaume na wanawake mnamo 2003,
(b) Aliyekuwa Raisi wa Amerika Bush mwana alisema katika dhifa nyingi kuwa Mungu alimzungumzisha na kumwambia afanye kadha na kadha. Hii ni licha ya kuwa Amerika ni dola ya kirasilimali na kimfumo inatakikana kutenganisha baina ya maisha na dini,
(c) Unyama uliotendwa katika jela za Abu Ghraib na Guantanamo mnamo 2003,
(d) Ufuatiliziaji wa Amerika wa maongezi ya simu, sio tu kwa raia wake, bali hata kwa Merkel na viongozi wengine,
(e) Hivi majuzi Theresa May aliulizwa ikiwa angetoa idhini ya shambulizi la kinyuklia linaloweza kuwaua maelfu ya wanaume, wanawake na watoto wasiokuwa na hatia. Alijibu "Ndio".

Urongo wa miito ya Kiamerika imewafanya Waamerika kuanza kuchukiwa ulimwengu mzima kutokana na serikali yao kuingilia mambo ya serikali zengine au nchi zengine. Hili limedhihirishwa kupitia maandamano ya mataifa yasiyo kuwa ya Kiislamu dhidi ya Raisi wa Amerika au dhidi ya maafisa wake wanao hudhuria makongamano au mikutano ya kimataifa. Kwa mfano:

(a) Mnamo 2014, kura ya maoni ilipigwa katika nchi 65, nchi marafiki na zisizo kuwa marafiki wa Amerika, na kura hizi zikatamatisha kuwa Amerika ni tishio kubwa la amani ulimwenguni,
(b) Mnamo Machi 2016, Raisi wa Cuba Raul Castro aliukukuta mkono wa Obama baada ya kumaliza mkutano wa pamoja wa waandishi habari mjini Havana, Cuba.
(c) Mnamo Septemba 2016, Barack Obama alilazimika kutoka kwa mlango wa nyuma wa ndege alipo zuru China kwa sababu Wachina hawaku muandalia ngazi zenye zulia jekundu la heshima,
(d) Barack Obama alifutilia mbali mkutano wake na Raisi wa Ufilipino Rodrigo Duterte mjini Laos kwa sababu alimuita Obama mtu aliye laaniwa,
(e) Miezi michache iliyopita, watu walio kuwa na hasira jijini Brussels waliandamana kupinga ziara ya Trump huku wakiwa na michoro ya vinyago vyake vikiwa na pua ndefu kuashiria kuwa ni mtu mrongo.

Ama kuhusu hali ya ndani nchini Amerika, haina afadhali. Kwa mfano:

(a) Mnamo 2011, na kwa mara ya kwanza katika historia ya Amerika, waandamanaji (walio zingira barabara ya Wall Street) walilalamika na kutaka kubadilisha mfumo wa kirasilimali,
(b) Mnamo 2012, zaidi ya majimbo 15 ya Amerika yaliomba kujitenga kutokana na serikali ya majimbo ya Amerika,
(c) Mnamo 2016, watu walikusanyika dhidi ya ghasia kwa watu weusi,
(d) Punde baada ya kutangazwa Trump kuwa Raisi, watu waliandamana wakibeba mabango yaliyo andikwa "Wewe si raisi wangu".

2. Amerika, nchi ya kwanza duniani, imefeli kijeshi nchini Afghanistan na Iraq na kutokana na haya, kupoteza nguvu zake nyingi za kijeshi licha ya kuwa Afghanistan ni nchi dhaifu na Iraq ni nchi waliyokabidhiwa. Hili ni wazi kutokana na matamshi ya amiri jeshi mkuu Ray Odierno aliye sema, "Jeshi letu kwa sasa liko katika kiwango cha chini

Endelea Uk..6

sana kimatayarisho tangu nianze kulitumikia muda wa miaka 37 iliyopita." Pia, katika Makala ya tarehe 16 Julai 2017 katika jarida la National Interest Magazine, Douglas Macgregor, kanali mstaafu, alisema, "Jeshi liko katika ukingo wa kupoteza pesa zaidi endapo Raisi Trump hata teua waziri mwenye nguvu na maarifa kwa jeshi hili – mtu ambaye atakuwa tayari kuwahisabu kwa lazima majenerali wake na kuitisha mabadiliko kamili. Litashindwa katika mapigano ya kwanza katika vita vinavyo kuja. Na, katika karne hii ya ishirini na moja, Waamerika hawatapata fursa nyengine ya kupigana vita vya pili."

Hili limeleta athari mbaya kwa Waamerika wenyewe ambapo siku hizi hufikiria mara elfu moja kabla ya kuamua kutuma vikosi vyake sehemu nyengine za ulimwengu wa Kiislamu. Hili lime dhihirika nchini Libya mnamo 2011 ambapo Amerika haikutuma vikosi vyake nchini humo, bali ilishiriki tu kijuu juu katika mashambulizi ya angani kupitia muungano wa NATO.

Kwa upande mwengine, hapana budi kuzingatiwa kuwa nguvu ya kijeshi haipimwi kwa idadi ya wanajeshi au silaha (Umoja wa Kisovieti uliporomoka huku ukiwa na hazina kubwa ya silaha) bali hupimwa kwa ari na kujitolea. Kwa mfano, wanajeshi wa Amerika nchini Iraq walidhani kuwa wako likizoni na kwamba hatimaye watarudi kwa familia zao na kupokea malipo yao ya kimada na kuishi maisha yao yaliyo bakia raha mustarehe, lakini hali haikuwa hivyo. Wanajeshi wa Amerika nchini Iraq walifikia hatua ya kuvaa vibinda kutokana na hofu ya kutoka ndani ya vifaru vyao kukabiliana na mahitaji yao, bila ya kutaja wale waliorudi kwa familia zao huku wakilalamikia maradhi mabaya ya msongo wa mawazo.

3. Mgogoro wa kifedha wa kiulimwengu ulikuwa ni risasi ndani ya moyo wa Amerika (na ulimwengu). Mgogoro huu wa kifedha umeidhoofisha athari ya Amerika (ya moja kwa moja au isiyo kuwa ya moja kwa moja) kwa Waislamu na watawala wa Waislamu, na kupelekea pia udhaifu kwa watawala hawa kibinafsi na kwa huduma zao za usalama kwa watu wao. Hususan gharama kubwa za kijeshi inazotumia Amerika kwa kambi 737 za kijeshi za Kiamerika zilizoko ndani ya nchi 130 ikiongezewa na kambi 6000 zilizoko ndani ya Amerika, zinazo hitaji pesa nyingi mno, pamoja na gharama za vita vya kiulimwengu dhidi ya ugaidi, usaidizi kwa majeshi ya kigeni, kufadhili miradi mengine itokanayo na bajeti ya umma ya Kiamerika, na gharama za vita vya muda mrefu vya Iraq na Afghanistan.

Walter Andrusyszyn, profesa wa biashara ya kimataifa katika Chuo Kikuu cha Florida Kusini, alisema "Deni kubwa la Amerika haliumizi tu uchumi wetu, linadhoofisha pia usalama wetu wa kitaifa na kuufanya ulimwengu kuwa mahali pa hatari zaidi. Hakuna taifa linaweza kudumisha au kudhihirisha nguvu yake ikiwa uchumi wake ni dhaifu. Hii ni kwa Sparta (Ugiriki ya kale), Roma, na Amerika."

Hivyo basi, idara iliyopo sasa ya Amerika imeamua kupunguza usaidizi wake wa kimaendeleo kwa asilimia 30, itakayo kuwa na athari mbaya kwa Amerika kwani misaada hii hukadiriwa kuwa moja ya nguzo tatu zinazo changia katika uwepo wa Amerika duniani, mbali na ulinzi na diplomasia. Zaidi ya hayo, hivi majuzi, Trump alizuru Saudi Arabia na kuchukua utajiri wa umma kwa njia isiyoeleweka.

Kutokana na yote hayo ya hapo juu, Amerika haina uwezo wa kushinikiza suluhisho la kisiasa kwa Mashariki ya Kati, iwe ni Syria au Afghanistan au kwengineko. Ni wazi kuwa, siasa ya kigeni ya Amerika leo inaporomoka. Kwa mfano, Trump alibadili maoni yake juu ya NATO kuwa ni muungano uliopitwa na wakati, kama alivyouita, na kisha kugeuza msimamo wake huu hadharani. Pia alijiondoa kutoka kwa makubaliano ya hali ya anga ya jijini Paris, na kisha kuitisha majadiliano mapya, alisimama katika ukingo wa vita na Korea Kaskazini, na kisha kurudi nyuma. Zaidi ya hayo, alikuwa na mtazamo mbaya juu ya China, na hatimaye kusimama nayo huku akisubiri matokeo ya faili yake nchini Korea Kaskazini, alitoa taarifa kali juu ya ardhi ya Syria, na kisha kuziachia mambo yake Astana na Geneva ambazo ni majirani zake.

Kwa haya na mengine mengi, yamemfanya Fukuyama kuzingatia upya fikra zake awali kuhusu Mwisho wa Historia. Zaidi ya hayo, haishangazi kumuona Raisi Obama akisoma kitabu kwa jina "Ulimwengu Baada ya Amerika".
Kwa mukhtasari, yote yaliyo tangulia juu yanathibitisha kuwa Amerika inazidi kudhoofika. Zbigniew Brzezinski amethibitisha haya alipo sema, "Amerika bado ni dola iliyo na nguvu zaidi kisiasa, kiuchumi na kijeshi duniani lakini, kutokana na mabadiliko makubwa katika mizani ya siasa za kimaeneo, sio tena serikali iliyo na nguvu za kipekee duniani."

Kuanguka kwa Amerika kumesababisha kuibuka kwa mafahali wengi wa kimfumo baada ya kuwa fahali alikuwa ni mmoja tu akiwakilishwa na Amerika baada ya kuporomoka kwa Umoja wa Kisovieti. Lakini habari njema kwa umma ni kuwa hakuna yoyote kati ya mafahali hawa aliye na nguvu za kutosha kama inavyo fafanuliwa hapo chini.

4. Ama kuhusu Ulaya, Ulaya kuitwa "kikongwe" imethibitika leo. Udhaifu wao ukokatika kushindwa kwao kutenda kimataifa, kugongana kwao kimaslahi na kuwepo kwa sera tofauti tofauti zinazo pelekea kuwepo na migongano katika kadhia nyingi.

Kwa mfano, huku Ujerumani ikienda dhidi ya sera za Amerika, Ufaransa inajikaribisha kwa Amerika, ilhali Uingereza bado haina uhakika kuhusu kujiondoa katika Muungano wa Ulaya.

Bila ya kutaja udhaifu wa Ulaya kutokana na mgogoro wa kifedha wa kiulimwengu, uliouweka Muungano wa Ulaya katika hali mbaya sana.

***Endelea Uk..7***

Kwa upande mwengine, kupungua kwa viwango vya watoto wanao zaliwa pamoja na vijana imepelekea kurudi nyuma kwa wakaazi wa Ulaya kisiasa na kiuchumi na kuhatarisha muelekeo wa bara hili kimikakati.

5. Umoja wa Kisovieti, uliyo kuwa dola ya pili kinguvu ulimwenguni umeporomoka.

Ama kuhusu Urusi, haina tena nguvu kama zile ilizokuwa nazo Umoja wa Kisovieti. Hili ndilo linalo elezea sababu kwa nini Urusi inajiuza kwa thamani ndogo katika kuisaidia Amerika nchini Syria huku ikishindwa kuizuia Amerika kuingilia majirani zake kama Ukraine au kuiondolea vikwazo ilivyowekewa na Amerika.

6. Ama kuhusu China, ingawa imeibuka kuwa na nguvu kiuchumi na kuwa na jeshi lenye nguvu, hili peke yake halitoshi kuiwezesha kuipiku Amerika kuwa dola inayoongoza duniani. Licha ya hayo, kuinuka kwa China na kuongezeka kwa mvutano kati ya Amerika na China kwaweza kuwa na manufaa kwa umma na kuzaliwa kwa Khilafah.

Ama kuhusu kuamka kwa Ummah:

Allah (subhanahu wata'ala) asema:

أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَىٰ قَرْيَةٍ وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا قَالَ أَنَّىٰ يُحْيِي هَٰذِهِ اللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ بَعَثَه

Au kama (mfano wa) yule aliye pita katika mji ulio kwisha kuwa magofu, akasema: Allah ataufufua vipi mji huu baada ya kufa kwake? Basi Allah akamfisha muda wa miaka mia. [al-Baqara: 2: 259]

1. Kukita mizizi kwa Uislamu nyoyoni mwa Waislamu ni jambo lililo dhihirika licha ya majaribio makali kufanywa ili kuwaweka mbali Waislamu na Uislamu wao. Mifano yake inapatikana nchini Uzbekistan, Iraq, Tunisia na Syria ambako watawala wake wametawala kimabavu kuwaweka mbali Waislamu na Uislamu, lakini mbali na hayo wameshindwa katika majaribo yao.

2. Utekelezaji Uislamu kibinafsi ni jambo lililo enea leo, ambapo haikuwa hivyo miaka 70 na kitu iliyo pita. Kuswali, kusoma Qur'an, kutazama vituo vya runinga za kidini, na uvaaji hijab yote yanajitokeza leo duniani. Picha iliyo chapishwa na kituo cha Al-Jazeera ya barabara ya Misri iliyo pigwa katikati mwa karne iliyopita ikilinganishwa na picha ya barabara hiyo hiyo iliyo pigwa miaka michache iliyopita ni mfano mzuri wa kushikamana na Uislamu kibinafsi.

3. Fikra za ujamaa, ukomunisti na utaifa pamoja na al-Nasiriyah na fikra nyenginezo zimethibitika kuwa za kimakosa akilini mwa Waislamu. Na yeyote anaye endelea kuzibeba fikra hizi ni lazima sasa ajizibe kwa Uislamu ili akubalike. Mifano ya haya ni mapinduzi ya Iran, kufuga ndevu kwa mfalme Husain, kesi ya Erdogan, demokrasia kugeuzwa kuwa Shura na kampeni za uchaguzi katika biladi nyingi za ulimwengu wa Kiislamu nk.

Hata matukio nchini Algeria, Misri, Syria na biladi nyenginezo pia ni mifano mizuri ya Waislamu kutaka Uislamu pekee.

Mfano mwengine ni wa raia wa Libya aliyejeruhiwa (kwa sababu ya vita) katika hospitali za Jordan alipokataa kuisalimisha bendera ya Rayah (waliyo kabidhiwa na wanachama wa Hizb ut Tahrir wakati Hizb ilipowatembelea mahospitalini) kwa huduma za kijasusi za Jordan na kuwaambia kwamba Rayah hii ndio sisi (Walibya) tunayo pigana kwa ajili yake nchini Libya.

Zaidi ya hayo, tukiweka udadisi wa kisiasa kando kwa sasa, fikra ya kuweka amani na kidola cha kiyahudi ilitoweka wazi wazi wakati ulipo tokea moto mkubwa mnamo Novemba 2016. Hii yathibitisha kuwa kuweka amani na "Israel" ni wino tu katika karatasi lakini umma wangependa kuona kumalizika kwa kidola hiki.

4. Jihad kwa ajili ya Allah imekuwa ndio matakwa ya vijana wa Kiislamu baada ya kukanyagwa kwa Waislamu Palestina, Iraq, Afghanistan, Bosnia, Kashmir, Chechnya, Somalia, Libya na Syria. Vile vile, mama za mashuhadaa katika nchi zote hizi wamesimulia upya hadithi kubwa zinazo fanana na zile za wanawake wakongwe wa Kiislamu kama vile Al Khansa'. Na kadhia ya hivi majuzi ya milango ya Jerusalem (Al-Quds) ni mfano mzuri wa haya. Ni muhimu kuzingatia pia kuwa mashuhadaa hao walikuwa ni vijana na Waislamu wa "kawaida" ambao hawaonyeshi kushikamana na dini kwa mtazamo uliozoeleka na watu. Kwa hivyo, Waislamu wanapoa kutokana na maradhi aliyotuonya nayo Mtume (saw) alipo sema,

حُبُّ الدُّنْيَا وَكَرَاهِيَةُ الْمَوْتِ

Kupenda dunia na kuchukia mauti.

5. Huku tukizingatia kuwa nguvu za kijeshi za Amerika zimeharibiwa nchini Afghanistan na Iraq na kwamba nguvu za kijeshi za "Israel" ziliharibiwa mnamo 2006, Waislamu kwa jumla na haswa maafisa wa kijeshi wameanza kutambua kwamba wanaweza kuwashinda wamagharibi na washirika wao, awe ni Bashar au Iran au Urusi maadamu watamtegemea Allah (subhanahu wata'ala) peke yake.

6. Baadhi ya maafisa wa kijeshi na wanajeshi wa Kiislamu wamefanya vitendo murua kabisa kudhihirisha kheri iliyomo ndani yao. Nchini Misri, Sadat aliuwawa na Waislamu wenye imani. Nchini Jordan, mwanajeshi aliwapiga risasi na kuwaua watalii wa kiyahudi kwa sababu walikuwa wakimkejeli alipokuwa akiswali. Nchini Syria, huduma za kijasusi zilikuwa zikiwahoji maafisa wengi wa kijeshi kwa kutozijulisha kuwa walipokea simu kutoka kwa Hizb ut Tahrir mnamo 2005. Nchini Sudan, afisa wa jeshi wa ngazi ya juu aliangika bendera ya Rayah, aliyo kabidhiwa na ujumbe wa Hizb ut Tahrir, juu ya kambi yake ya kijeshi. Nchini Yemen, mmoja wa wanajeshi ilijipiga risasi mguuni mwake ili asiweze kushiriki katika mauaji ya raia wa Kiislamu, na kadhalika.

7. Wamagharibi walirudi kuja kuzikoloni biladi za Kiislamu kijeshi mnamo 2001 na 2003. Hili lenyewe

*Endelea Uk..8*

ni ishara kuwa umma bado uko hai, na kama si hivyo ni kwa nini basi wamagharibi wapigane na taifa ambalo limekufa hususan ikiwa tayari wanatawala siasa, uchumi, vyombo vya habari na mitaala yetu ya elimu na kadhalika? Kwani wamagharibi watakuwa wanaogopa kitu gani? Wamagharibi wanaogopa kurudi kwa Khilafah. Ushahidi wa haya ni:

(a) Raisi Bush, mnamo Oktoba 11, 2006, alisema kuwa kuwepo kwa Amerika nchini Iraq kulikuwa ni kwa ajili ya kuzuia kusimama kwa Khilafah.
(b) Henry Kissinger, aliye kuwa Waziri wa Kigeni wa Amerika, aliandika Makala yaliyo chapishwa katika gazeti la 'International Herald Tribune Newspaper' mnamo 2 Aprili 2012, akifafanua kuwa sera ya Amerika kwa dini yetu imejengwa juu ya nguzo mbili: kudumisha (uporaji wa) mafuta na kuhifadhi "Israel". Lakini, akasema kwa sasa tunaongezea nguzo ya tatu nayo ni kuzuia kuibuka kwa dola yoyote katika eneo itakayo liunganisha eneo zima chini yake.
(c) Lavrov, Waziri wa Kigeni wa Urusi, amesema kuwa kuporomoka kwa Assad itamaanisha kuibuka kwa serikali ya kisunni; bila shaka, hamaanishi serikali ya kisunni mfano wa Jordan na Saudi Arabia.

8. Mapinduzi ya Kiarabu yaliyofanyika katika baadhi ya sehemu za ulimwengu wa Waislamu yalikuwa na natija kadhaa nzuri:
(a) Yaliutia nishati Umma wa Kiislamu na kunyanyua hisia ya kujiamini kwake,
(b) Yalivunja kizingiti cha hofu,
(c) Yalidhihirisha umoja wa Umma huu,
(d) Yaliwatweza mashekhe-pesa pamoja na fikra ya kila mtu ajibadilishe kibinafsi,
(e) Yalimakinisha zaidi utambuzi kuwa tatizo la Umma liko katika viongozi (yaani ni vipi kivuli kitakuwa wima ikiwa kijiti hakiko wima),
(f) Yaliinua matakwa ya Waislamu kulingania Khilafah kama ilivyo kuwa nchini Yemen, kukusanyika mamilioni ya watu wakitaka sharia kama ilivyo kuwa nchini Misri, kupambana na viongozi wa kiilmani kama ilivyo kuwa nchini Tunisia, kupiga takbira "Allah Akbar" kama ilivyo kuwa nchini Libya, na kutoa kauli za "Peponi tutakwenda, tukiwa mamilioni ya mashuhadaa", "Ewe Allah hatuna mwengine isipokuwa Wewe", na "Tunamsujudia Allah peke yake" kama ilivyo kuwa nchini Syria.
(g) Mashekhe wengi nchini Misri, Saudi Arabia, Kuwait, Yemen, Jordan na nchi nyenginezo wakaanza kuhutubia kuhusu Khilafah Rashida ya pili.

Hivyo basi, uhalisia wa mapinduzi haya ya watu yaliobarikiwa ukajitokeza, licha ya kuwa vyombo vya habari vilijaribu kuuziba uhalisia huu. Na muamko wa Kiislamu unaendelea kukua.

9. Ripoti kadhaa zilitolewa na Wamagharibi zinazo onyesha uungaji mkono wa Waislamu kurudi tena kwa Khilafah, ripoti hizi ni kama:

(a) Ripoti iliyo tabiri kuwa kufikia mwaka wa 2020 Khilafah itakuwa imesimama tena.
(b) Kura ya maoni iliyo fanywa na shirika la Amerika la Gallup, zilizo onyesha kuwa idadi kubwa ya Wamisri wanaunga mkono kutawala kwa Sharia na kwamba thuluthi mbili ya Wamisri wanataka kuifanya Sharia iwe ndio chimbuko pekee la kanuni.
(c) Ripoti ya Maryland inaonyesha kuwa Waislamu nchini Pakistan, Indonesia, Morocco na Misri wanapendelea Sharia badala ya demokrasia.

Hii ndio maana Wamagharibi wakaitumia ISIS kama hatua ya mwisho kuwapotosha Waislamu kutokana na ulinganizi wa Khilafah. Lakini, kwa rehma za Allah (swt), siku baada ya siku, Khilafah ya ISIS imethibitika kuwa maneno matupu angani.

Ama kuhusu maendeleo ya Hizb ut Tahrir:

1. Kuna wabebaji da'wah wamakinifu wanaofanya kazi kwa hili. Na ulinganizi wowote, kujitokeza kwa uhakika wake, huwa ni suala la wakati tu maadamu wapo walinganizi wanao ufanyiakazi. Na Alhamdulillah da'wah ya Hizb ut Tahrir imeenea kutoka Australia upande wa mashariki mpaka Amerika upande wa magharibi. Zaidi ya hayo, Alhamdulillah, Hizb imeweza kuwaathiri wasomi, vyama, na watu wengi kiasi ya kuwa mamia ya kurasa hayatoshi kuwanakili.

Kuenea huku kukubwa kwa Hizb kumezighadhabisha nchi za kimagharibi, kufikia hatua ya, kwa mfano, kufanywa kongamano la siku mbili nchini Uturuki mnamo Septemba 2004 kwa anwani: "Changamoto ya Hizb ut Tahrir: Kuelewa na Kupambana na Mfumo Wenye Msimamo Mkali wa Kiislamu" lililodhaminiwa na kituo cha Kiamerika cha Nixon Center. Natija za kongamano hilo zilinakiliwa katika ripoti ya kurasa 157.

2. Hizb imefafanua fikra zote za Kiislamu zinazo husiana na Khilafah na ubebaji ulinganizi wake katika hali ambayo imewafanya Waislamu kurudisha imani yao kwa Uislamu, kufikia hatua kwamba Chama cha Kikomunisti katika Muungano wa Kisovieti kiliwaambia wafuasi wake nchini Palestina/Jordan kutofanya mazungumzo yoyote na Hizb kutoka na ufahamu wao mzito.

Hizb pia ilijitofautisha na vyama vyengine vya Kiislamu kupitia kutayarisha katiba kielelezo mpaka kufikia hatua kwamba mmoja wa viongozi wa chama cha 'Islamic Salvation Front' nchini Algeria wakati mmoja aliwahi kuulizwa: ikiwa mutapata mamlaka ya kutawala, je munayo katiba tayari kuitekeleza? Jibu lake lilikuwa, tunayo katiba ya ndugu zetu katika Hizb ut Tahrir. Kwa hivyo, Hizb iko tayari sana kwa Khilafah kiasi ya kuwa hata mitaala ya shule iko tayari.

3. Hizb imeshikamana barabara na fikra na njia yake, licha ya yale wanayo yapitia wanachama wake katika mateso ambayo wakati mwengine hupelekea mpaka kufikia daraja ya ushahidi, huku wanachama

*Endelea Uk..9*

wa vyama vyengine wakiwa dhaifu mbele ya mmomonyoko wa kisiasa na kifikra au hata mbele ya fimbo na karoti. Zaidi ya hayo, fikra na njia ya Hizb zimethibitishwa kuwa sahihi wakati wa mapinduzi ya kiarabu, hususan kuhusiana na suala la kutafuta nusra kwa watu wenye nguvu, ambapo harakati nyengine ziliikejeli Hizb kwa hilo.

4. Hizb ilifaulu kuharibu uhusiano kati ya watawala na watu. Huku watu wengi wakiwatetea watawala hawa kama vile Arafat, Nasser, Saddam na wengineo, na huku baadhi ya harakati kubwa za Kiislamu zikikosa kuona madhara ya kuanzisha mahusiano ya kirafiki na watawala hawa, Hizb ilikuwa ikiwapiga vita watawala hawa kisiasa kufikia kiwango ambapo maraisi wa Uzbekistan na Pakistan, kwa mfano, walilalamika kuhusu Hizb ut Tahrir kwa Uingereza.

5. Hizb ilifanya makongamano kadhaa muhimu, kama kongamano la wasomi, la kiuchumi, la vyombo vya habari, na makongamano kadhaa ya wanawake, ambapo vyombo vya habari havikuwa na budi isipo kuyaangazia. Haya ni kuongezea maandamano ambayo Hizb ilifanya kabla ya harakati zote nyengine, yote yakidhihirisha historia ndefu ya Hizb, yakiwemo yale yaliyofanyika nchini Jordan kuunga mkono watu wa Syria na Libya na lile lililofanyika nchini Indonesia mnamo Machi 2017 ambapo watu milioni tatu walikusanyika dhidi ya gavana wa Jakarta aliye itusi Qur'an na Uislamu.

6. Hizb ut Tahrir imeomba na inazidi kuomba nusra kutoka kwa watu wenye nguvu walioko katika nchi kama Jordan, Syria, Misri, Iraq, Pakistan na kwengineko. Muitikio mzuri kwa Hizb kutoka kwa baadhi ya watu wenye nguvu unajulikana vyema na kutajwa wazi katika vyombo vya habari.
Mwisho, matukio haya na hali hizi zinazotoa njia ya kuzaliwa kwa Khilafah hayapaswi kutufanya tuzubae na kusubiri, bali yanapasa kuwatia motisha, kuwashajiisha na kuwachangamsha wale ambao tayari wanafanya kazi au wale ambao wangependa kufanya kazi kusimamisha Khilafah Rashida ya pili. Hivi ndivyo walivyo kuwa maswahaba wa Mtume Muhammad (saw) wakizifanyia kazi bishara njema. Mtume (saw) alibashiri kufunguliwa kwa mji wa Kostantiniyya; maswahaba hawakusubiri tu kutimia kwa ahadi ya Mtume wa Allah pasi na kuifanyia kazi, bali walijaribu mara kadhaa ili kupata tunu ya kuufungua mji huu mpaka ulipoweza kufunguliwa na Mohammed Al Fateh (Mfunguzi). Vile vile, Hizb ut Tahrir imeamua, kama walivyo fanya maswahaba wa Mtume (saw), kuendelea kufanya kazi na Ummah na kwa ajili ya Ummah, mpaka wakati ule ambao Allah ataamuru kusimama tena Khilafah katika njia ya Utume utakapo wadia.

فَسَيُنْغِضُونَ إِلَيْكَ رُءُوسَهُمْ وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هُوَ قُلْ
عَسَىٰ أَن يَكُونَ قَرِيبًا

**Watakutikisia vichwa vyao, na watasema: Iini hayo? Sema: 'asaa yakawa karibuni!** [Qur'an 17:51]

**Imeandikwa na Ghassan Kaswani**
**Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Ni Nani Atakaye Komesha Mauaji ya Halaiki Dhidi ya Waislamu wa Rohingya?

**Hotuba ya Dkt. Nazreen Nawaz, Mkurugenzi wa Kitengo Cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir (Iliyotolewa nje ya Ubalozi wa Bangladesh, Jijini LondonTarehe 9 Septemba 2017)**

**Kaka na Dada zangu wapendwa,**

Kama mujuavyo, Waislamu wa Rohingya katika jimbo la Rakhine nchini Myanmar kwa sasa wanakabiliwa na kampeni katili ya mauaji ya halaiki mikononi mwa serikali katili ya Myanmar, wanaandamwa kwa kisingizio cha urongo cha kupambana na ugaidi. Jinamizi hili ambalo ndugu na dada zetu wa Rohingya wanateseka nalo halielezeki. Kwa muda wa wiki mbili sasa, wanajeshi wa Myanmar na wakaazi walio jihami kwa silaha wa dhehebu la Budha wamekuwa wakitekeleza mauaji ya kinyama dhidi ya Waislamu wa Rohingya – wamekuwa wakiwamiminia risasi kiholela wanaume,wanawake na watoto, kuteketeza nyumba zao na vijiji vyao, wakiwakata kwa visu na mapanga raia wasiokuwa na hatia hadi kufa – yote kwa sababu tu wanasema "La-ilaha illallah...Mungu wangu si mwengine isipokuwa Allah!".

Mamia ya ndugu zetu na dada zetu na watoto wao wameuwawa. Video za kuogofya za wanawake na watoto wakiuliwa kinyama na wauwaji hawa wa kibudha zimekuwa zikizunguka katika mitandao ya kijamii. Misikiti na Madrassa zimechomwa mpaka kuwa jivu. Na kwa uchache Waislamu wa Rohingya wapatao 270,000 wamekimbia Myanmar na kuelekea Bangladesh kutafuta hifadhi (kwa kukisia hii ni thuluthi moja ya Waislamu wote wa Rohingya wanaoishi Myanmar) – asilimia 80 yao wakiwa ni wanawake na watoto kulingana na shirika la UNICEF, huku maelfu wakiwa wamekwama bila ya chakula wala makao. Madazeni ya wanawake na watoto wa Rohingya wamekufa maji wakijaribu kukimbilia Bangladesh kwa mashua. Mlinzi wa mpakani wa Bangladesh alituma picha kwa shirika la CNN zinazo onyesha maiti za watoto wadogo zikitapakaa katika fuo za Mto Naf. La hawla wala quwatta illah billah!

Majeshi ya usalama ya Myanmar yamekuwa yakiwarushia maguruneti na risasi raia wanao kimbia na kujaribu kuvuka mpaka kuingia Bangladesh kutafuta hifadhi, na hivi majuzi kumekuwa na ripoti kuwa jeshi la Myanmar linatega mabomu ya ardhini katika mpaka

*Endelea Uk..10*

wa Bangladesh kuwazuia wakimbizi wa Rohingya kutorudi, ambayo yamesababisha majeruhi mabaya kwa baadhi ya watoto wa Rohingya. Hasbunallah wa ni'mal wakeel!

Ripoti hizi zilizo ibuka kutoka Myanmar za mauaji haya ya halaiki dhidi ya ndugu zetu na dada zetu wa Rohingya na magaidi hawa wa kibudha kwa kweli ni za kuchukiza. Watoto wa Kiislamu kuchinjwa na wengine shingo zao kunyofolewa au kutupwa ndani ya maziwa, akiwemo mtoto mchanga wa miezi sita. Wanaume wa Kiislamu wakikusanywa na kutiwa ndani ya nyumba ya miti ya bamboo kisha kuwashwa moto na kuteketezwa hadi kufa.

Na yote haya ni miongoni tu mwa matukio mapya ya mauaji ya halaiki ambayo Waislamu wa Rohingya wanakumbana nayo katika miongo kadhaa ya mateso nchini Myanmar, ambapo dada zetu wamenajisiwa na magengi na kutazama watoto wao wakichinjwa mbele ya macho yao. Miongo ya kuishi katika uovu wa ubaguzi na umasikini uliokithiri, wakinyimwa haki msingi za elimu, huduma za afya na ajira, wakilazimishwa katika ndoa na sheria za kiimla za uzazi ili kudhibiti idadi yao, na kunyimwa uraia na serikali katili ya Myanmar, kuwapelekea kutokuwa raia wa serikali yoyote katika ardhi ambayo wameishi kwa vizazi na vizazi.

Hivyo basi nawauliza ndugu zangu na dada zangu, ni nani atakaye komesha mauaji haya ya halaiki dhidi ya Waislamu wa Rohingya? Ni serikali ipi iliyoko leo duniani itakayo jitokeza na kumaliza umwagaji damu huu? Ni serikali ipi iliyoko leo duniani yenye hisia ya maadili mema kusimama dhidi ya serikali ya Myanmar na kuwatetea Waislamu wa Rohingya, kuweka maisha ya wanadamu juu ya maslahi ya kisiasa au ya kiuchumi? Ni serikali ipi iliyoko leo duniani inayowakilisha kweli maslahi ya Waislamu ambayo itatia hofu ndani ya nyoyo za jeshi la Myanmar na makatili wa kibudha kiasi ya kuwa hawata subutu kumdhuru hata Muislamu mmoja wa Rohingya mwanamume, mwanamke au mtoto?

Tunajua wazi kuwa HAKUNA serikali aina hiyo, hakuna mfumo aina hiyo, hakuna taasisi yoyote ya kimataifa ulimwenguni leo itakayo weza kufanya haya kwa sababu tumeshuhudia mauaji ya halaiki nchini Syria…na ulimwengu haukufanya lolote; mauaji ya halaiki ya Waislamu nchini Afrika ya Kati… ulimwengu haukufanya lolote; mauaji ya halaiki ya Waislamu wa Kashmir, Somalia, Afghanistan, na kwengineko… ulimwengu pia haukufanya lolote!

Kaka na dada zangu, leo, kila serikali ulimwenguni inayaona mauaji haya ya halaiki, inasikia vilio vya wanawake na watoto wasio kuwa na hatia, inashuhudia udhalimu mbaya na mateso ya viwango visivyo elezeka…lakini inageuza macho yake, na kuosha mikono yake kutokana na jukumu lolote la kulinda maisha ya wasiokuwa na hatia… kwani kwa maoni yao… na kulingana na mfumo wao wa kinyama wa KIRASILIMALI… kuyaokoa maisha haya hakuna pato la kisiasa wala la kiuchumi ndani yake. Kisha eti wanadai kuwa DEMOKRASIA ni ustaarabu huku Sheria ya Kiislamu inayo wajibisha serikali inayo tawala kwayo kulinda wanadamu kutokana na unyama na udhalimu wa madhalimu, ni ya kikatili! Subhaanallah!

Kunyamaza kimya, na hata kukana kwa Aung San Suu Kyi, kiongozi wa kiimla wa Myanmar, na shabiki mkuu wa demokrasia, kuwepo na umwagaji damu huu na kampeni ya kinyama ya kikabila dhidi ya Waislamu na jeshi la nchi hiyo…na kwamba hali ni kama kawaida kwa serikali za kidemokrasia ulimwengu mzima katika mahusiano yao na serikali katili ya Myanmar… inafichua wazi kwa mara nyengine tena sura halisi ya nidhamu ya kibinadamu ya kidemokrasia ambapo dhulma na uchinjaji wa wasiokuwa na hatia hupuuzwa endapo maslahi yataamua.

Na kaka na dada zangu, kuhusu muitiko wa serikali na watawala katika ulimwengu wa Kiislamu juu ya mauaji haya ya halaiki dhidi ya Waislamu…muitikio wao umekuwa upi? Hali hii ni ya kuchukiza mno! Serikali ya Hasina nchini Bangladesh, badala ya kuwakaribisha Waislamu hawa wanaoteseka katika fuo zake na kuwapa hifadhi, bali imewaamuru walinzi wake wa mipakani kuwafurusha kutoka mipakani mwake…na kuwaacha wakifa maji katika mashua zao mbovu au kurudi katika ardhi ya mauaji ya Myanmar, au imewachukuwa na kuwaweka katika kambi duni zisizo kuwa na mahitaji msingi, na kukataa kuwatambua kama wakimbizi.

Maelfu ya Waislamu wa Rohingya wamekwama katika ardhi isiyomilikiwa na serikali yoyote katikati ya mpaka baina ya Myanmar na Bangladesh. Mapema mwaka huu, serikali ya Hasina ilifikiria hata kuwaondoa wakimbizi wa Rohingya na kuwapeleka katika kisiwa kilichoko sehemu ya chini eneo la Bengal ambacho hukumbwa na mafuriko ya mara kwa mara ambacho kimepewa lakabu ya 'kisiwa kisicho kaliwa' na mashirika ya kutetea haki. Subhaanallah! Lakini khiana ya Hasina imeongezeka zaidi, kwa kuwa serikali yake inapendekeza oparesheni ya pamoja na serikali katili ya Myanmar kusaidia ile inayoitwa oparesheni 'dhidi ya ugaidi', kwa jina jengine, kampeni ya mauaji ya halaiki dhidi ya Rohingya. *La hawla wala quwatta illah billah*!

Serikali khaini ya Pakistan pia haina uchungu wowote kuhusu kuongezwa nguvu zaidi jeshi katili la Myanmar na kudhulumu kwa kuwachinja kaka zao na dada zao wa Kiislamu. Mnamo 2015, ilitia saini mkataba wa kupeleka ndege kumi na sita za kivita aina ya JF-17 kwa jeshi la Myanmar, licha ya mauaji ya halaiki ya Rohingya yaliyotokea mnamo 2012. Ndege hizi zinatarajiwa kuanza kutumika kwa mara ya kwanza na jeshi la anga la Myanmar mwaka huu.

*Endelea Uk..11*

Na vipi kuhusu serikali ya Saudi Arabia, serikali za ghuba, Misri, na Jordan? Ziko tayari kutumia nguvu zao za kijeshi kuuwa na kuwanyima chakula watoto wa Yemen kwa kutii maagizo ya mabwana zao wa kimagharibi kuliko kutumia majeshi yao kuwaokoa watoto wa Kiislamu wa Myanmar!

Na vipi kuhusu Uturuki? Uturuki ambayo ni nchi ya saba kwa ukubwa wa jeshi ulimwenguni na ya pili kwa nchi za NATO… ni upi muitikio wa uongozi wake katika mgogoro huu? Raisi wake, Erdogan alichagua tu kujihusisha na hatua nyepesi ya kidiplomasia na kiongozi Suu Kyi, ikiwemo kumuomba ruhusa ya kupeleka misaada kwa Rohingya iliyo athirika na ghasia hizi. Subhaanallah! Kiongozi wa ardhi ambayo mwanzoni ilikuwa makao makuu ya dola kuu ya Khilafa, dola iliyokuwa na nguvu zaidi duniani iliyo wafanya maadui wa Uislamu kutetemeka kwa hofu… leo anaona haja ya kuomba ruhusa serikali inayo wauwa Waislamu kuwapelekea misaada wale wanao kimbia kichinjo cha serikali hiyo hiyo?! Subhaanallah! Hii inadhihirisha kiwango kikubwa cha idhlali ambayo viongozi wa Waislamu wamefikia leo!

Wakati huo huo Waziri wa Kigeni wa Uturuki alitoa wito kwa Bangladesh kufungua milango yake kwa wakimbizi wa Rohingya wanaokimbia ghasia, huku akisema kuwa Uturuki italipia gharama zote za mahitaji yao…akijaribu kujionyesha shujaa katika mkasa huu kwa njia ya kejeli. Tuna mwambia Erdogan na serikali yake…vipi kuhusu kuyaachilia huru majeshi yako kutokana na kuyatumikia maslahi ya serikali za kimagharibi na NATO na kuyashajiisha katika lengo lao halisi… kulinda damu ya Waislamu nchini Myanmar na ulimwengu mzima, kusimama dhidi ya wanao watesa Waumini, kuwaokoa kutokana na wauwaji wao…na kulipia GHARAMA ZOTE YA HAYA?! Erdogan alisema, "Wale wanao yafungia macho mauaji haya ya halaiki na kuendelea kufanya hivyo chini ya pazia ya demokrasia wote ni washirika kwa hili" – sisi tunasema – ndio Erdogan – hili ni kweli – linalo kufanya wewe na biladi zote za Kiislamu pia kuwa washirika katika uhalifu huu mkubwa…kwani nyote mumekaa kimya ilhali munaweza kusitisha umwagaji huu wa damu kupitia majeshi yenu!

Ni tofauti kubwa ilioje kati ya serikali hizi ovu za watawala Waislamu na vijana na mabinti watiifu wa Ummah huu waliojitokeza barabarani kwa wingi katika kila nchi ulimwenguni, (kutoka Indonesia mpaka Pakistan. Bangladesh mpaka Malaysia, na kwengineko, ikiwemo hapa Uingereza ambapo leo kutakuweko na maandamano nje ya Ubalozi wa Bangladesh jijini London yatakayo hudhuriwa na Waislamu kutoka kila pembe ya Uingereza). Wamejitokeza kudhihirisha uungaji mkono wao kwa kaka zao na dada zao Waislamu wa Rohingya na kuzitaka serikali za Waislamu kukata mahusiano na serikali katili ya Myanmar na kukomesha umwagaji damu huu. Serikali hizi zisizo na chembe ya uchungu hazistahili kutawala juu ya Ummah huu mtukufu hata kwa sekunde moja… zinahitaji kung'olewa…kwani Ummah huu unastahili uongozi utakao dhihirisha mapenzi kwa kaka na dada zake Waislamu kwa ajili ya dini yake.

Kaka na dada zangu wapendwa, hakuna serikali leo itakayo komesha umwagaji damu huu dhidi ya kaka na dada zetu Waislamu wa Rohingya… kwa hivyo ni juu yetu sisi, Ummah wa Rasulillah (saw) KUKOMESHA mauaji haya ya halaiki. Ili kufanya hivyo…haitoshi tu kuhisi uchungu na kumwaga machozi tunapoona yale yanayo endelea kwa kaka na dada zetu, au hata kuonyesha hasira, au hata kuwaombea dua tu. Ni lazima tuunganishe uchungu na hasira zetu kwa SULUHISHO lilio fafanuliwa na dini yetu litakalo komesha jinamizi hili kwao!

Na SULUHISHO hili ni kufanya kazi kusimamisha serikali iliyo na hisia ya maadili mema kusimama dhidi ya uhalifu huu muovu kwa wanadamu; serikali itakayo wakilisha kweli maslahi ya Waislamu na dini yetu; serikali ambayo kiongozi wake ame wajibishwa kuwa mlinzi wa Ummah huu na damu yake; serikali ambayo jeshi lake litakumbatia dori yake halisi ya kuwa mtetezi kwa Waislamu;  NA serikali ambayo NIDHAMU YAKE YA KIISLAMU itatoa himaya, maisha yenye hadhi na haki kamilifu za Uislamu kwa uraia kwa Waumini walio dhulumiwa bila ya kujali wanakotoka.

Serikali hii kaka na dada zangu, si nyengine isipo kuwa ni KHILAFAH katika njia ya utume, nidhamu ya Allah (swt), kwani, hakika Mtume (saw) amesema,

إِنَّمَا الْإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ

**Hakika Kiongozi (Imam) ni ngao, watu wanapigana nyuma yake na wanajihifadhi kwake.**

Kwa hivyo, tunawalinganienі enyi kaka na dada zetu kutoa juhudi zenu zote katika ubebaji wa da'wah hii ya kusimamisha serikali ya Khilafa Rashidah ili tukomeshe uchinjaji huu wa Ummah wetu nchini Myanmar na ulimwengu mzima na kurudisha izza kwa Waumini na kwa dini yetu. Fanyeni kazi na sisi kama Hizb ut Tahrir kusimamisha serikali hii tukufu ambayo haitapumzika mpaka kila serikali dhalimu ibadilike kuwa historia na haki itawale katika dunia hii.

Na kwa maafisa wa kijeshi Waislamu katika ulimwengu wa Kiislamu, tuna walingania kuitikia vilio vya kaka zenu, dada zenu na watoto wenu Waislamu wa Rohingya wanao waomba kuja kuwahifadhi. Ukombozi wao uko mikononi mwenu. Musifuate njia ya watawala wenu walio andaliwa makaazi yao Jahannam kwani wame wakhini Waislamu na dini hii. Toeni nusra (nguvu za kijeshi) yenu haraka iwezekanavyo kwa uongozi shujaa wa Hizb ut Tahrir kusimamisha serikali ya Khilafa itakayo wahamasisha mara moja kuhifadhi damu ya Ummah wenu, na kuufanya urithi wenu ule unao fanana na wa mashujaa wakubwa katika dini hii mfano wa Salahuddin Ayubi na Muhammad ibn Qasim… na kuwaletea heshima katika maisha

*Endelea Uk..12*


haya ya duniani na ujira mkubwa kesho Akhera.

Na Allah (swt) asema,

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَـٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ ٱلرِّجَالِ وَٱلنِّسَآءِ وَٱلْوِلْدَٰنِ ٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَآ أَخْرِجْنَا مِنْ هَـٰذِهِ ٱلْقَرْيَةِ ٱلظَّالِمِ أَهْلُهَا وَٱجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيًّا وَٱجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيرًا

**Na muna nini musipigane katika njia ya Allah na ya wale wanao onewa, miongoni mwa wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola wetu! Tutoe katika kijiji hiki ambacho watu wake ni madhalimu, na tujaaliye tuwe na mlinzi anaye toka kwako, na tujaaliye tuwe na wa kutunusuru anaye toka kwako.** [An-Nisa: 75]

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo Cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 5: Kumrai/Kumbembeleza Mtume (saw) awache Da'wah

Hapo awali tulisema kuwa Maquraysh walitumia mbinu nne dhidi ya da'wah ya Mtume (s.a.w). Katika Halaqa hii tutaangazia mbinu ya kwanza nayo ni kumbembeleza Rasulullah (saw) awache da'wah.

Katika harakati za kujaribu kumzuia Mtume (saw) awache da'wah, Maquysh waliamua kumtuma Abal Waleed Utbah bin Rabia kama balozi kwa Mtume (saw) ambembeleze na akawa anamwambia:

"Ewe Muhammad hakika wewe unajua kwetu sisi una nafasi katika nasaba,na ni wa kati na kati (unaetambulika) katika jamaa,na hakika watu wanaona kuwa wewe umekuja na jambo kubwa. Umeutenganisha umoja wao, na ukawafanya wajinga werevu wao, na ukaaibisha miungu yao na dini yao ukawakufurisha waliotangulia katika wazee wao.Hakika wamekusanyika watu watukufu katika jamaa zako, nao wamekubaliana nikuelezee mambo,uyaangalie, huenda ukakubali miongoni mwayo baadhi yake ama ukapendezwa na yote."

Mtume (saw) akamwambia Utbah: "Sema ewe Abal Waleed,mimi nasikia."

Akasema Utbah:
"Ewe mtoto wa ndugu yangu,ikiwa unataka kwa haya uliokuja nayo mali tutakukusanyia mali mpaka uwe mwenye mali nyingi zaidi yetu! Na ikiwa wataka cheo tutakufanya wewe ndiye bwana wetu mpaka tusikate shauri/maamuzi kando na wewe. Na ikiwa wataka ufalme tutakufanya uwe mfalme wetu. Na ikiwa haya yanayokujia ni ndoto za kishetani,huwezi kujikinga nazo nafsi yako tutakutafutia tiba na tutoe mali yetu mpaka tukupoze au tushindwe. "

Utbah alipomaliza kusema;
Rasulullah (saw) akamuuliza: "Ushamaliza ewe Abal Waleed?" Utbah akajibu "ndio". Mtume (saw) akamwambia: "Basi nisikilize nami." Akajibu Abal Waleed: "Nitakusikiliza..."

Rasulullah (saw) akasema yafuatayo:

حَم ، تنزيلٌ مـِنَ الرَّحمَن ِالرَّحيم ِ، كِتابٌ فـُصِّـلـَتْ آيَاتـُهُ قـُرآنـا ً عَرَبيَّا ً لِلقـَوم ٍ يَعلمُونَ ، بـَشيرا ً وَنذيرا ً فأعْرَضَ أكثرُهُمْ فـَهُممْ لا يَسمَعُونَ ، وَقـَالـُوا قـُلـُوبُنا فِي أكِنـَّةٍ مِمَّا تـَدعُونـَا إليـهِ وَفي آذانِنـَا وَقر ٌوَمِنْ بَينـِنـَا وَبَينـِكَ حِجَابٌ فاعمَـلْ إنـَّنـنـَا عَامِلـُونَ

H'a Mim. Uteremsho huu umetoka kwa Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.
Hichi ni Kitabu kilicho pambanuliwa Aya zake, cha kusomwa kwa Kiarabu kwa watu wanaojua. Kitoacho khabari njema, na chenye kuonya. Lakini wengi katika wao wamepuuza; kwa hivyo hawasikii. Na wakasema: Nyoyo zetu zimo katika vifuniko kwa hayo unayo tuitia, na masikio yetu yana uziwi. Na baina yetu na wewe lipo pazia. Basi wewe tenda, nasi tunatenda.

[Fussilat: 1 – 5]

Kisha Mtume (saw) akaendelea kumsomea Suratul Fussilat na alipoisikia Utbah alinyamaza kuisikiliza na akaiegemeza mikono yake nyuma akimsikiliza Mtume (saw). Mtume (saw) alikomea katika Aya ya sajdah. Nayo ni kauli yake Allah (swt):

وَمِنْ آياتِهِ الليلُ وَالنـَّهارُ وَالشمسُ وَالقمَرُ لا تـَسجُدُوا لِلشمس ِوَلا لِلقمَر ِوَاسجُدُوا للهِ الذي خـَلقـَهُنَّ إنْ كـُنتـُمْ إيَّاهُ تعبُدُونَ

Na katika Ishara zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu aliye viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu.
[Fussilat: 37]

Mtume (saw) baada ya kusujudu kisha akamwambia: "Umesikia yale uliyoyasikia, basi ni wewe na hayo uliyoyasikia."

Baada ya hapo Utbah akasimama na kuelekea kwa watu wake. Watu wake walipomuona Utbah wakawa wanaambiana kuwa tunaapa na Allah hakika amewajieni Abal Waleed kwa uso ambao hakuenda

*Endelea Uk..13*

nao. Alipokaa nao wakamuuliza:"Ni kipi kilicho nyuma yako ewe Abal Waleed? akajibu,"Nyuma yangu hakika nimesikia maneno,WALLAHY sijasikiapo mfano wake.WALLAHY si mashairi,wala uchawi wala ukuhani...!!Enyi mkusanyiko wa Maquraysh,nitiini mimi na munibebeshe mimi jukumu hili na muondoke kati ya huyu mtu na kati ya yale aliyonayo,mwacheni. WALLAHY ,itakua kwa maneno niliyoyasikia kwake, khabari kubwa. Waarabu wakimsibu basi itakua mumetoshelezwa na wengine. Na akiwashinda Waarabu,basi ufalme wake ni ufalme wenu na izza yake ni izza yenu,na mutakua ni wenye saada zaidi kupitia kwake..."

Baada ya hapo wakaenda Maquraysh kwa ammi yake Mtume (saw), Abu Taalib ili amzuie Rasulullah (saw) na da'wa ili awaridhishe Maquraysh na mabwana wao. Basi haikua kwa Mtume (saw) ila alimpa majibu ambayo kwamba hayakubali maelewano wala suluhisho la kati na kati na kuwajibu:

"Ewe ammi,WALLAHY lau wataeka jua katika mkono wa kulia na mwezi katika mkono wangu wa kushoto ili niwache hili jambo sitoliwacha mpaka Allah alidhihirishe ima nife.

Kisha Maquraysh wakamtaka Mtume (saw) awawachie mushrikina kwa baadhi ya waliyo nayo naye Mtume (saw) awache baadhi ya aliyo nayo. Ikateremka raddi/jawabu kutoka kwa Allah (swt):

ودوا لو تدهن فيدهنون

Wanatamani lau unge lainisha ili nao wakulainishie.
[Al-Qalam:9]

Wakamtaka Rasulullah (saw) aabudu miungu yao kwa mwaka na wao wamuabudu Mola wake kwa mwaka. Wakajibiwa na Allah (swt):

قل يآ أيهاالكافرون¤لاأعبدماتعبدون

Sema: Enyi makafiri! Siabudu mnachoabudu
[Al-Kaafiroon: 1 – 2]

Allah (swt) akamaliza ubembelezaji wao wa kuchekesha kwa fafanuzi hizo za kukata au moja kwa moja.

Yalipofeli majaribio yote yaliyotangulia ambayo Maquraysh waliazimia ili kumuondosha Mtume (saw) katika da'wah yake. Walikwenda katika mbinu nyengine miongoni mwa mbinu chafu za ubembelezaji (kati na kati)! Wakambembeleza Mtume (saw) wamuamini kwa sharti asiwataje miungu yao kwa uovu akakaribia Rasulullah (saw) kukubali akiwa na tamaa ya kusilimu kwao na akidhani kuwa hili halita dhuru da'wah, lakini usaidizi wa kiungu, upole na uchungaji wa kirabbaaniya kwa hii da'wah ulimpatiliza. Kwani Mtume (saw) hakuamka kutoka kwa kikao hicho cha ubembelezaji mpaka akamjia Jibril (as) kwa kauli yake Allah (swt):

وَإِنْ كادُوا لَيَفتِنُونَكَ عَنِ الذي أوحَينَا إليكَ لتفتريَ
عَلينَا غيرَهُ إذاً لا تَّخذوكَ خلِيلاً ، وَلَولا أنْ
ثَبَّتنَاكَ لقَدْ كِدْتَ تتركَنُ إليهمْ شَيئاً قليلاً ، إذاً
لأذقْنَاكَ ضِعفَ الحَيَاةِ وَضِعْفَ المَمَاتِ ثُمَّ لا تَجِدُ
لكَ عَلينَا نَصِيراً .

Na hakika walikaribia kukushawishi uache tuliyo kufunulia ili utuzulie mengineyo. Na hapo ndio wangeli kufanya rafiki. Na lau kuwa hatukukuweka imara ungeli karibia kuwaelekea kidogo. Hapo basi bila ya shaka tungeli kuonjesha adhabu mardufu ya uhai, na adhabu mardufu ya kifo kisha usingepata mtu wa kukunusuru nasi.
[Al-Israa: 73-75]

Hakika utetelekaji wowote uwe ni mdogo kwa mbebaji da'wah, hata kama utetelekaji huo ni sehemu katika sehemu za da'wah, basi huwa ni utetelekaji katika da'wah yote. Kwani kila kifungu miongoni mwa vifungu vya ubebaji da'wah huwa ni mfano wa kifungu chengine, nayo ni hukmu ya kisheria miongoni mwa hukmu za twariqa. Inatakikana kusimama nayo wala haijuzu kuteteleka kwayo kabisa.

Itaendelea Katika UQAB Toleo 10… In Shaa Allah.

# SWALI / JAWABU:
## Mkakati wa Amerika Nchini Afghanistan

**Swali:** mnamo Agosti 15, 2017, kundi la Taliban lilituma barua ya wazi kwa Raisi wa Amerika likitoa wito wa kuondolewa kwa majeshi ya Amerika kutoka Afghanistan, na kutoongeza majeshi ya Amerika: "Harakati ya Taliban ilitoa wito kwa Raisi Donald Trump kuondoa majeshi yake yote kutoka Afghanistan, na kumuonya katika barua ya wazi dhidi ya kuongeza idadi ya vikosi vya Kiamerika ndani ya nchi hii iliyoshindwa kudhibitiwa na Washington…" (Chanzo: Novosti – RT – Russia Today, 15/8/2017). Haya yamejiri kujibu dhamira ya Trump ya kuweka mkakati mpya nchini Afghanistan, ambao Taliban inahofia utahusisha utumaji wa vikosi vipya, huku taarifa kutoka kwa maafisa wa ikulu ya white house zikisisitiza kuwa mkakati huu utakuwa hivi karibuni. Tovuti ili nukuu taarifa ya Trump kwa wanahabari mnamo 10/8/2017: kuwa idara yake iko 'karibu sana' ya kuamua mkakati mpya kwa Afghanistan… aliongeza: "Ni maamuzi makubwa sana kwangu. Nilirithi vurugu na tutajaribu kupunguza vurugu lake". Je, ina maana kuwa Amerika iko makini juu ya kuunda mkakati mpya nchini Afghanistan? Je, itahusisha kutuma vikosi vipya au itahamasisha Pakistan au dori ya India nchini Afghanistan pasi na kutuma vikosi vipya vya Kiamerika? Jazakum Allah Khair.

Endelea Uk..14

**Jibu:** Ndio, yaweza kusemwa kuwa leo Amerika ina regelea upya kwa umakinifu mkakati wake nchini Afghanistan na pengine yaweza kupata muongozo kwa kile inachokiita 'hatua ya mwisho' ya kuingilia kati kwake nchini Afghanistan. Trump ameghadhabishwa na uongozi wa jeshi nchini Afghanistan. Shirika la wanahabari wa kimataifa liliripoti mnamo 3/8/2017 mkutano mkali ulio fanyika kati ya Raisi wa Amerika, Trump, na maafisa wa kijeshi wa Amerika jijini Washington. Kulikuwa na mvutano mkali wakati wa mkutano huo ambapo Trump alisema kuwa Waziri wa Ulinzi James Mattis pamoja na kinara wa jeshi Joseph Dunford ni lazima wajadiliane kuhusu kumuondoa Jenerali John Nicholson, kamanda wa jeshi la Amerika nchini Afghanistan, kwa kushindwa na vita. Kwa hivyo, Trump ameonyesha tashwishi zake juu ya vita vya Amerika nchini Afghanistan. Idara ya Obama pia ili regelea na kufanya marekebisho mkakati wa Amerika nchini Afghanistan, lakini urekebishaji wa idara ya Trump leo ni wa kipekee kwa sababu umetokea katika mazingira ambapo matatizo ya kimataifa yameongezeka kwa Amerika na nafasi yake ya kiulimwengu; ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

**Kwanza:** Amerika ilitangaza vita vyake kwa Afghanistan mwishoni mwa mwaka wa 2001 chini ya visingizio vya kujibu shambulizi la Septemba 11, vikiongozwa na wanaharakati wanaotetea maslahi ya Amerika ya kimataifa kupitia matumizi ya nguvu za kijeshi (neo-conservatives) walio kuwa wameizunguka idara ndogo ya Bush. Baada ya miaka chini ya miwili, Amerika ikaishambulia Iraq, na kuikalia, ilizama ndani ya mchanga wake na hatimaye kutafuta usaidizi wa kujikwamua. Kupitia kushindwa kwa Amerika nchini Iraq, vita vyake nchini Afghanistan vikapungua umuhimu wake, na ikaanza kuelekeza juhudi zake juu ya kujiondoa kutoka kwa janga la Iraq na upinzani wa Iraq ukawa ndio wasiwasi mkubwa kwa idara ya Bush na baadaye idara ya Obama. Kupitia kufaulu kwa idara ya Obama kuondoa vikosi vingi vya kijeshi vya Amerika kutoka Iraq mwishoni mwa 2011, Amerika sasa imeamua mkakati mpya wa kupambana na kuinuka kwa China. Kadhia hii ilitawala awamu ya pili ya idara ya Obama na kabla ya mkakati wa Amerika kukamilishwa na hata wakati wa kutayarishwa na kumakinishwa kwake, athari ya Amerika katika eneo la bara Arabu ilitingishwa na msururu wa mapinduzi ya kiarabu, hususan nchini Syria. Amerika imeendelea kueneza juhudi zake za kupambana na hatari za mapinduzi ya bara Arabu, hususan Syria pamoja na kupambana na China eneo la Mashariki ya Mbali.

Amerika ilitangaza kukataa kwake visiwa vya kichina na kufanya kazi kufufua jeshi la kijapani na kuanza kuichokoza Korea Kaskazini. Kwa sababu ya hili na kwa sababu majeruhi wa Kiamerika nchini Afghanistan hawakuwa mahututi, vita vya Amerika nchini Afghanistan vilipewa umakinifu mdogo na Amerika ingawa hili halimaanisha kuvipuuza kabisa licha ya kuwa Amerika imejishughulisha zaidi na vipaumbele vipya.

**Pili:** Wakati wa vita vya muda mrefu vya miaka 16 nchini Afghanistan, yaweza kusemwa kwa njia ya kukatikiwa kuwa Amerika na majeshi ya NATO, iliyo shiriki nayo katika vita, yalifeli vibaya mno kung'oa upinzani kwa Kiafghani, kimsingi Taliban, iliyo banduliwa mamlakani mnamo 2001 kwa uingiliaji kati wa Amerika. Inawezekana pia kusisitiza kuwa hatua zote za Kiamerika za kumakinisha vibaraka wake nchini Afghanistan pia zimefeli; India, ambayo Amerika ili itambulisha kwa Afghanistan kwa lengo la kuzuia kile Amerika inacho kiita uasi, haikuifaidisha. Kuongezea, haikufaidika sana kutokana na vita hivi, vilivyo chochewa na vibaraka wake nchini Pakistan katika eneo la Waziristan na kwengineko, kujaribu kupunguza hasara za Amerika nchini Afghanistan, na hakukuwa na maendeleo yoyote katika juhudi za upatanishi na Taliban. Kwa hivyo, hali ya Amerika nchini Afghanistan bado ni tete hata baada ya miaka 16 ya vita. Taliban inatembea ikiwa huru katika maeneo mengi ya Afghanistan, na serikali kibaraka ya Kabul haina athari yoyote juu yake. Harakati hii inatekeleza mashambulizi ya nguvu na ya kuogofya katika eneo kubwa la Afghanistan, ikiwemo Kabul, ambako jeshi la Amerika halija faulu kumakinisha usalama, lakini mashambulizi mengi, ambayo yametekelezwa dhidi ya majeshi ya Amerika, yalifanywa na wanachama wa jeshi la Afghan walio funzwa na Washington; hivyo basi, hatua za Amerika nchini Afghanistan ni hafifu.

Katika ufafanuzi wake wa uhakika wa Afghanistan leo na hatari zake, ripoti ya shirika la Carnegie Endowment for International Peace (22/5/2017) ilisema "… mkusanyiko wa serikali dhaifu ya Afghan na uasi usio dhibitiwa wa Taliban unaweza kupelekea janga la kuporomoka kwa serikali ya nchi ya Afghanistan, itakayo pelekea ima kurudi tena kwa machafuko au kuzuka tena kwa makundi ya kigaidi." Ripoti hiyo inasisitiza kwamba mgogoro wa Afghan lazima umalizike sio tu kwa sababu unaigharimu Amerika dolari bilioni 23 kwa mwaka, bali kwa sababu ya hatua hafifu kwa suluhisho la Afghanistan.

Licha ya kuondoka kwa majeshi mengi ya Amerika kutoka Afghanistan chini ya Raisi Obama, na kubaki vikosi 10,000 pekee, vikisaidiwa na vikosi 3,000 vya NATO pamoja na vikosi 20,000 kutoka kwa kampuni za usalama za Amerika, kujiondoa huko hakukutokana na ushindi wowote au maendeleo yoyote. Taliban ilizikalia kambi zilizo achwa wazi na jeshi la Amerika kwa haraka, na serikali kibaraka ya Afghan haionekani kufanya kazi barabara nje ya jiji kuu la Kabul licha ya idadi yake kubwa na licha ya juhudi nyingi za Amerika kuipa mafunzo; hii ikiwa ni katika upande wa kijeshi.

**Tatu:** Katika upande wa kijeshi, baada ya Amerika kutambua udhaifu

*Endelea Uk..15*

wa hatua zake nchini Afghanistan na kufilisika kwa hatua ya India, ili amua kufuata njia ya majadiliano na Taliban kwa matarajio ya kuijumuisha ndani ya serikali kibaraka ya Afghanistan, na ime watumia vibaraka wake katika serikali ya Pakistan kuwashurutisha viongozi wa Taliban kuingia katika majadiliano. Lakini, majaribio yote hayo yamefeli; Amerika haikufaulu kijeshi wala kisiasa juu ya kadhia ya Afghanistan, bali Amerika hana mpango maalum juu ya kadhia hii, na amekashifiwa kwa kukosa mpango aina hiyo nchini Afghanistan. Shirika la Interfax Agency mnamo Alhamisi lili nukuu kutoka kwa Wizara ya Kigeni ya Urusi ikisema kuwa kushindwa kwa idara ya Raisi Donald Trump kuwasilisha sera wazi wazi juu ya Afghanistan ni jambo linaloongezea zaidi shauku na ukosefu wa utulivu ndani ya nchi hii, ikiongeza kuwa uwepo wa majeshi yake unategemea kiwango cha nguvu za serikali ya Afghan na msimamo wa nchi wanachama wa NATO, na matarajio ya kutuliza hali nchini humo kwa jumla. (Russia Today, 3/8/2017).

**Nne:** Kina cha mgogoro wa Amerika nchini Afghanistan kiko wazi sasa, na udhaifu wa hatua zake pia uko wazi, iko katika haja kubwa ya kupunguza joto la vita vya Afghanistan lau ikiwa haita wezekana kuvimaliza kabisa ili kuzuia kufilisika kwa uwezo wake wa kijeshi na kiuchumi. Baadhi ya viongozi wa kijeshi wanaona haja ya kuongeza wanajeshi wa Amerika ili kushinda vita dhidi ya Taliban. Trump anataka mpango huo uwe wa muda mfupi, na uwe na natija ya wazi na thabiti kama sharti la kukubali hilo ambapo jeshi haliwezi kutoa hakikisho kwalo kutokana na hisia chungu lilila nayo juu ya Afghanistan kwa muda wa miaka 16. Kinacho ifanya hatua hii kuwezekana tu kinadharia ni kule kuwa mdomo wa Trump unamwaga nyute za ulafi kutokana na utajiri mkubwa wa madini wa Afghanistan, unaokadiriwa thamani yake kuwa dolari trilioni moja, pamoja na kuwa ndio mkondo wa mafuta kutoka Asia ya Kati. Tovuti ya gazeti la Al-Dustour, mnamo Julai 26, 2017, ilinukuu jarida la New York Times: "Katika hali ya kutafuta uwezekano, ikulu ya White House ina kadiria kutuma mjumbe nchini Afghanistan kukutana na maafisa wa uchimbaji madini. Wiki iliyopita, huku ikulu ya White House ikizidi kutumbukia katika mjadala moto juu ya sera ya Afghanistan, watatu kati ya washirika wa bwana Trump walikutana na afisa mtendaji wa kemikali, Michael N. Silver, kujadili uwezo wa kuchimba madini nadra ardhini. Kampuni ya bwana Silver, American Elements, inajishughulisha na madini hayo, yanayo tumika katika utengezaji bidhaa za hali ya juu." Lakini hatua ya kutuma vikosi zaidi na kuwekeza katika muundo mbinu msingi wa Afghanistan, kama vile reli na barabara, ili kuwezesha uchimbaji madini hayo sio hatua salama hata kwa muangalio wa mipango ya kibiashara inayo tawala akili ya Raisi kutokana na uwezekano wa migodi hiyo kuangukia katika eneo linalo tawaliwa na Taliban.

Kutokana na hayo, hatua inayo tarajiwa zaidi kuchuliwa na idara ya Trump ni kuyaondoa majeshi ya Amerika kutoka katika kambi za kijeshi za Afghanistan ili kuimakinisha serikali kibaraka na kuzuia kuporomoka kwake, kwa kutia msukumo mkubwa kwa Pakistan kuregea kwake Afghanistan baada ya kufeli kwa India. Yote haya ni kwa lengo la kuishawishi Taliban kujiunga na nidhamu ya kisiasa ya Kiamerika jijini Kabul na kuzima mapinduzi ya Afghan; yaani, mwisho wa vita virefu zaidi vya Amerika. Hivyo basi, Amerika inatarajia kupunguza gharama za vita vyake nchini Afghanistan kupitia kuondoka kwake na badala yake kubakisha kambi zake za kijeshi, ili kumuwezesha kuchukua hatua pindi atakapo hisi tishio (sawa na kambi zake zilizoko eneo la Ghuba) na kuwasaidia vibaraka wake nchini Pakistan, ambao bado wana mafungamano na Taliban, na kwamba inawezekana kuyaimarisha zaidi mafungamano haya na kujenga imani ili Taliban ikubali masharti ya Amerika kupitia mlango wa Pakistan. Nyuma, Amerika ili watumia kwa mafanikio vibaraka wake wa Pakistan wakati wa utawala wa Obama: serikali ya Afghan ilifikia makubaliano na kundi la Kiislamu, kundi la pili kwa ukubwa nchini humo miongoni mwa makundi ya kisilaha, bila ya kuwepo kiongozi wake, Gulbuddin Hekmatyar, makubaliano hayo yalitiwa saini na wawakilishi wa kundi hili la kisilaha pamoja na Raisi Ashraf Ghani. (BBC, 22/9/2016). Jambo hili linaishajiisha Amerika kuitumia tena Pakistan juu ya kadhia hii ya Taliban hususan baada ya msimamo wa kimaridhiano wa Hekmatyar na kurudi kwake Kabul ambapo alitoa wito kwa Taliban kujiunga na nidhamu ya kisiasa. Kiongozi huyu wa kundi hili la Kiislamu nchini Afghanistan Gulbuddin Hekmatyar alitoa wito kwa Taliban kujiunga katika maridhiano na serikali ya Afghan, na kushajiisha harakati hii katika hotuba yake ya kwanza hadharani baada ya kuwasili kwake Kabul, kusaidia katika kuyatoa majeshi ya kigeni nje ya nchi kwa njia ya amani. (Al Jazeera.net, 6/5/2017)

**Tano:** Kutokana na hatari zinazo ikabili Amerika kutoka China, hususan hali inayozidi kuwa moto kati yake na Korea Kaskazini, matishio yanayo endelea nchini Syria, kufeli kwa sera zote za Kiamerika katika kuutibu uchumi wake, kuchoka kwa wanajeshi wa Amerika nchini Afghanistan, kukata tamaa ya kupata ushindi, kufisilika (kufeli) kwa dori ya India nchini Afghanistan na kuibuka kwa matarajio kupitia kurudi kwa Hekmatyar, yote haya ni matarajio ya wazi kwa Amerika kutaka kupatikana kwa maridhiano katika hali itakayo idhamini wakati ambapo vita vimeshindwa kuleta dhamana hii. Hii ndio maana iliamua kurudi na kufufua dori ya Pakistan nchini Afghanistan na kukomesha mashambulizi ya Pakistan ima ndani ya Afghanistan au katika mpaka wake na Afghanistan. Wakati wa uongozi mpya wa kijeshi, unaoongozwa na Bajwa, miezi minane iliyo pita, Pakistan imeachana na oparesheni zake kubwa kama zile za mtangulizi wake, Raheel Sharif, kwa mfano "Zarb-e-Azb" katika hatua kadhaa dhidi ya kile Raheel anacho kiita

*Endelea Uk..16*

“magaidi” katika mpaka wake na Afghanistan, badala yake, kumekuwa na ripoti za ghasia chache tu baina ya majeshi ya Pakistan na India katika mpaka wa Kashmir wakati wa uongozi wa Jenerali Bajwa. Na kwamba, hakuna shaka, hili linatilia nguvu uungwaji mkono wake kindani na katika ngazi ya vinara wa Taliban.

Kamanda mpya wa jeshi la Pakistan, Bajwa, alitaka kurefusha ushirikiano na Afghanistan chini ya mwito wa kupambana na kundi la ISIS; yaani, kutoa sura mpya fikra ya “vita dhidi ya ugaidi” kutoka kupigana na Taliban na Mujahidina wa Waziristan na badala yake kuelekeza vita kwa kundi la ISIS. Hii ikiwemo kuondoa chuki iliyokuwa nayo serikali ya Afghan na makabila ya Kiafghani dhidi ya mtangulizi wake, Raheel. Kilicho fichika katika mazungumzo kati ya Bajwa na Taliban-Afghanistan ni hatari zaidi: (Kamanda wa jeshi la Pakistan, Qamar Javed Bajwa, aliongeza ‘ushirikiano wa kiusalama’ na Afghanistan kukabiliana na tishio la ISIS katika hatua nadra za mahusiano kati ya nchi mbili hizi jirani. Jenerali Bajwa alitaka kuanzisha ushirikiano wa kiusalama na Afghanistan wakati wa mkutano wa Ijumaa na baadhi ya viongozi wa makabila ya bonde la Kurram, (kitengo cha kiidara kilichoko maeneo ya makabila ya Pakistan yanayo tawaliwa kimajimbo) karibu na mpaka wa Afghanistan. Kamanda huyu wa jeshi la Pakistan alitoa wito kwa nchi zote mbili, katika mahusiano nadra kati ya Pakistan na Kabul, “kuungana na kuwa macho”. Aliendelea kusema wakati wa mkutano wake na makabila hayo ya bonde la Kurram, “Ni lazima tuungane, tuwe tayari na tuwe macho dhidi ya tishio hili”) (Gulf Online, 1/7/2017)

Kinacho thibitisha kufeli kwa Amerika kuwashinda Mujahidina wa Kiafghani, hususan harakati ya Taliban, ni taarifa za maridhiano kutoka kwa Raisi wa Afghan baada ya kongamano la Trump nchini Saudi Arabia kwa kusema: “Kilicho muhimu zaidi ni kuwa serikali ya Afghan inataka maridhiano, na tunaomba Taliban ipewe khiari. Ikiwa watachagua maridhiano, watapata kila kitu kupitia siasa na sheria, na tunaomba Taliban isihusishwe na ugaidi.” (The Middle East, 25/5/2017). Hili linathibitisha kuwa sera ya Amerika inalenga kuionyesha Taliban kuwa ni kundi lililo nje ya upeo wa vita vya Amerika dhidi “ugaidi”, lakini sharti ijiunge na serikali ya Afghan katika vita hivi, na kwamba matakwa ya Taliban ya kuondolewa kikamilifu kwa vikosi vya Amerika kutoka Afghanistan yatapatikana kwa kupitia njia ya amani na wala si vita.

**Sita, na kutamatisha:** Mkakati wa Raisi Trump nchini Afghanistan umerekebishwa katika hali ambapo sera ya Amerika inakumbwa na tishio ulimwengu mzima. Kutokana na ukweli tulio tangulia kuutaja hapo juu, katika kurekebisha sera yake nchini Afghanistan, Amerika inatarajiwa kujumuisha yafuatayo:

1- Marekebisho haya yanafanywa kwa lengo la kupunguza joto katika ardhi ya Afghanistan, kudhibiti uwepo wa Amerika ndani ya kambi za kijeshi tu na kuzitumia wakati wa tishio. Na kubadili sura ya kandarasi yake kuwa ni dhidi ya kundi la ISIS pekee.
2- Haitarajiwi kuwa Amerika itatuma majeshi yake kwa lengo la kupigana na kuchochea, bali huenda ikatuma vikosi kwa muda mfupi tu na si kwa lengo la kupigana bali kwa lengo la kushajiisha karata ya majadiliano, kana kwamba Amerika yajaribu kusema inaweza “kulegeza msimamo” kupitia kuyaondoa majeshi haya ya ziada kwa kupitia Taliban pia “kulegeza msimamo” na kukubali kujadiliana na kugawanya mamlaka na serikali ya Afghan, na bila shaka, pasi na kugusa maslahi ya Amerika.
3- Ili kuharakisha kuivutia Taliban kukubali, Amerika itarudi kuimarisha dori ya Pakistan kupitia kuonyesha kuwa uongozi mpya wa kijeshi nchini Pakistan ni laini zaidi na wenye huruma kwa Taliban ili kuisukuma kuketi na kujadiliana na serikali kibaraka ya Kabul na kugawanya mamlaka katika nidhamu ya kisiasa ya Kiamerika nchini Afghanistan.

**Saba: na mwisho,** tunaonya dhidi ya kuwategemea vibaraka hawa nchini Pakistan au kuhakikishiwa kupitia ‘ulaini’ wa uongozi wao wa kijeshi kwa Afghanistan. Ni jukumu letu kujifunza kutokana na yaliyopita; Amerika haingetia mguu wake Afghanistan lau si usaidizi wa vibaraka wake ndani ya serikali ya Pakistan. Sera hii mpya ya serikali ya Pakistan dhidi ya Taliban ni mchezo tu unaochezwa na Amerika binafsi ili kukazanisha mchezo huo usiokuwa na lengo jengine ila kuondoa tishio zinazo mkambili kibaraka wake, serikali ya Afghanistan, pasi na kujitia gharama za uingiliaji kijeshi, au hata kwa gharama chache. Viongozi wapya wa Pakistan ni sura nyengine inayofichua mpango wa Amerika. Wakati mwengine, Amerika huwaagiza wafuasi wake nchini Pakistan kukaa ngumu dhidi ya Jihadi ya Kiafghani na kuivunjavunja, kama alivyo fanya jambazi Raheel katika Waziristan kulingana na mpango wa Obama. Na sasa watu wapya uongozini wanafanya kazi kuitongoza Taliban na kuidhibiti kulingana na mpango wa Trump, kutokana na kufeli kwa sera za Amerika za kuilazimisha kukaa katika meza ya hatari, “majadiliano”, kama njia ya kufuta ile ari ya Jihadi iliyo salia. Hivyo basi, wanajaribu kusukuma majadiliano kupitia mafungamano yao ya karibu kama njia ya kupotosha na kuhadaa, na tunaonya dhidi ya kuingia katika mitego ya Amerika na vibaraka wake au kuwategemea.

﴿وَلَا تَرْكَنُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُم
مِّن دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ﴾

**Wala msiwategemee wanao dhulumu, usije ukakuguseni Moto. Na wala nyinyi hamuna walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, wala tena hamtasaidiwa.** [Hud: 113]


Email: uqab@hizb.or.ke